# OFISI YA RAIS TAMISEMI
## HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

SHULE YA SEKONDARI MKUYUNI,
S.L.P 11605,
**MWANZA.**
TAREHE: .....

KUMB.NA MKY/SS/117/2021
Mwanafunzi: .....
S.L.P: .....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MKUYUNI WILAYA YA NYAMAGANA MKOA WA MWANZA – MWAKA 2021**

1.0 Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kuingia Kidato cha kwanza mwaka 2021 na hivyo kujiunga na Shule ya Sekondari Mkuyuni HONGERA ! Shule hii iko Kata ya Mkuyuni Jijini Mwanza.
Mhula wa masomo utaanza tarehe ..... unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ..... mwisho wa kuripoti ni tarehe ..... baada ya hapo utaipoteza nafasi yako.

**2.0 MAMBO YA MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 Sare ya shule:**

a) Sare ya Shule hii ni rangi **NYEUSI** sawa na kipande cha kitambaa kilichoambatanishwa. Unashauriwa kuwa makini ili kupata kitambaa halisi vinginevyo utalazimika kushona sare nyingine.

**Wavulana:**

- Suruali mbili si mdomo wa chupa wala mtepesho, yenye rinda mbili pande zote za mbele, mifuko miwili ya mbele na mmoja nyuma (isipokidhi viwango utalazimika kushona nyingine).

**Wasichana:**

- Sketi mbili zenye rinda box kushoto na kulia, mkanda wa tumboni uwe nchi mbili tu (isipokidhi viwango utalazimika kushona nyingine).
- Hijabu yenye rangi nyeusi isiyobana mwili (isipokidhi viwango utalazimika kushona nyingine).

b) Mashati mawili meupe yenye mikono mirefu, mfuko mmoja mbele upande wa kushoto yasiwe na mikanda mabegani kwa wavulana na wasichana pia (ukaguzi utafanyika)

c) Fulana ya rangi nyeupe kwa wavulana na shimizi nyeupe kwa wasichana (vitakaguliwa).

d) Viatu vyeusi vya ngozi (sio buti) vyenye visigino vifupi, soksi nyeupe ndefu zisizo na maua yeyote hadi usawa wa magoti kwa wasichana, wavulana watavaa soksi nyeusi (ukaguzi utafanyika).

e) Sweta – rangi ya kijivu yenye ufito mweupe mikononi na shingoni ni muhimu sana hasa majira ya baridi kali.

f) Track suti ya rangi nyeusi kwa wavulana na wasichana (zitavaliwa siku ya michezo tu – Ijumaa ya kila wiki).

NB. Sare ya Shule Kamili inapaswa Kuwa na nembo ya Shule.

## 2.2 VIFAA VYA TAALUMA:

- Daftari kubwa 11 (counter book Q.3) kalamu, mathematical set
- Ream 1 ya karatasi kwa matumizi ya mazoezi ya kitaaluma kwa mwaka mzima.

## 3.0 MWENENDO:

- Mwanafunzi ni lazima awe na heshima kwa walimu, viongozi, watu wazima na wazazi.
- Ni wajibu wa mwanafunzi kulinda na kutunza mali za shule. Upotevu au uharibifu wowote lazima ufidiwe.
- Mwanafunzi hataruhusiwa kutumia kilevi cha aina yoyote.
- Mwanafunzi hataruhusiwa kuwa nje ya shule kwa muda wa masomo au kwenda nyumba za walimu bila ruhusa maalumu.
- Ni marufuku mwanafunzi kuingia kwenye nyumba za starehe kama vile baa, disko na nyumba za kulala wageni.
- Ni wajibu wa mwanafunzi kutunza usafi wa mazingira ya shule pamoja na usafi binafsi.
- Mwanafunzi anapaswa kufika shuleni saa 1:00 asubuhi, kuhudhuria masomo yote na kutimiza majukumu yote aliyopangiwa na walimu au kiongozi.
- Ni marufuku mwanafunzi kujiunga na makundi ya uhalifu wa aina yoyote.
- Ni wajibu wa mwanafunzi kushiriki katika mipango ya shule bila uvivu au utoro.
- Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na kucha ndefu, nywele ndefu ama kusuka nywele.
- Mapambo juu ya sare ya shule hayaruhusiwi.
- Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu katika mazingira ya shule.

## 3.1 BAADHI YA MAKOSA YATAKAYOSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.

- Kudharau bendera ya Taifa
- Uasherati, ushoga, usagaji na ubakaji.
- Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
- Makosa ya jinai au kufikishwa mahakamani
- Kupata mimba, kutoa mimba au kusababisha ujauzito.
- Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- Kuwa na simu ya mkononi shuleni.
- Wizi
- Kupigana
- Kuoa au kuolewa
- Utoro uliokithiri
- Kugoma au kuongoza vurugu
- Kukataa adhabu halali kwa makusudi

## 3.2 VIAMBATANISHO:

1. Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga wa hospitali ya serikali, fomu ikabidhiwe kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
2. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki lkatika migomo, fujo na makosa ya jinai.
3. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria na maelekezo mengine halali kama yatolewavyo na shule.
4. Pamoja na viambatanisho (1-3) unatakiwa kuja na kivuli cha cheti cha kuzaliwa siku ya kuripoti shuleni.

KARIBU SANA

.....

**MWITALE BP**
**MKUU WA SHULE**

Picha

# HABARI ZA MWANAFUNZI

Mimi ..... (jina la mwanafunzi) nakubaliana na maagizo yote yaliyoelekezwa katika baura ya kujiunga niliyopewa na shule. naahidi kwamba, kwa muda wote nitakaokuwa hapa shuleni, nitatii na kuyatekeleza kwa dhati, kinyume chake nitakuwa sijajielimisha na kutumiza wajibu wangu.

Na ya kwamba nitakuwa tayari kumfikisha mzazi/mlezi taarifa yoyote ihusiyo maendeleo yangu ya taaluma na mwenendo na ama kumfikishia wito wa kufika shuleni pindi ahitajikapo kufanya hivyo.

Endapo nitakiuka maagizo ya shule ama kuvunja sheria za shule kuwa namna yoyote ile, oungozi wa shule utachukua jukumu la kuniondoa shuleni au kunisimamisha masomo

Naahidi pia nitajielimisha kadri ya wezo wangu na kwamba nitaitumia elimu hiyo kwa manufaa ya wananchi wenzangu wote.

Jina la mwanafunzi: .....
Sahihi ya mwanafunzi: ..... tarehe .....
Jina la mzazi/mlezi: .....

## TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina lako ..... (jina hili halitabadilishwa kwa muda wote utakapokuwa hapa shuleni)
2. **Baba**
   - i. Jina la Baba yako: .....
   - ii. Yu hai/amefariki: .....
   - iii. Anuani yake: ..... namba ya simu: .....
   - iv. Kazi na cheo chake: .....
   - v. Dini ya Baba: .....
3. **Mama**
   - i. Jina la mama yako: .....
   - ii. Yu hai/amefariki: .....
   - iii. Anuani yake: ..... Namba ya simu .....
   - iv. Kazi na cheo chake: .....
   - v. Dini ya mama yako: .....
4. Mlezi: (mlezi ni mtu asiye mzazi wako, lakini anakutunza na kukuhudumia kwa chakula na mahitaji mengine)
   - i. Jina la mlezi huyo ni: .....
   - ii. Uhusiano wako na mlezi(mjomba, kaka, rafiki, shangazi, baba mdogo nk).....
   - iii. Anuani ya mlezi wako: .....namba ya simu.....
   - iv. Kazi ya mlezi wako ni: .....

Picha

# HABARI ZA MZAZI/MLEZI

Mimi .....mzazi /mlezi wa ..... makazi yangu ni mtaa wa .....

**a. Ahadi**

Naahidi kwamba, nitashirikiana na uongozi wa Shule katika malezi ya mwanangu muda wote awapo Shuleni, nitafatilia mahudhurio yake ya siku zote za masomo na mwenendo wake wa kitaaluma. Hivyo, nitakuwa tayari kuitika miito yote ya Shule ikiwa ni pamoja na kufuata maelekezo yote halali yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa Shule.

**b. Mashauri.**

Kwa masuala yote ya mashauri yanayohusu mwanangu, wafuatao pia watahusika;-

| 1. | 2 | 3 |
|---|---|---|
| picha | Picha | Picha |
| Jina ..... | Jina ..... | Jina ..... |
| Uhisiano ..... | Uhusiano ..... | Uhusiano..... |

| | | |
|---|---|---|
| c..... | ..... | ..... |
| Jina la mzazi/mlezi | Sahihi | Namba ya simu |
| d..... | ..... | ..... |
| Jina la Mtendaji wa Mtaa | Sahihi na mhuri | Namba ya simu |

Form No. 1

# THE PRESIDENT'S OFFICE - RALG
# MWANZA CITY COUNCIL
# MKUYUNI SECONDARY SCHOOL P.O.BOX 11605 MWANZA

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF A STUDENT SELECTED TO JOIN FORM ONE YEAR 2021.

The medical officer

.....

.....

.....

Name of pupil: .....

Please examine the above mentioned as to his/her fitness for Secondary Education according to the following items below;-

| NO | ITEM | CONDITION | REMARKS |
|---|---|---|---|
| 1 | Mental condition | | |
| 2 | Sight | | |
| 3 | Hearing | | |
| 4 | Chest TB | | |
| 5 | Urine | | |
| 6 | Stool | | |
| 7 | Nose | | |
| 8 | Blood BP, HB | | |
| 9 | Pregnancy test | | |

Any other physical disability not listed that may affect his/her studies

.....

.....

In my opinion the student is fit/to join secondary school education

SIGNED: .....

MEDICAL OFFICER: .....

OFFICAL STAMP: